# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**Mtaa wa Mwenge,**
**S.L.P. 588,**
**54201 Mbozi - Songwe.**
**Simu: (025) 2580226**
**Nukushi: (025) 2580213**
**Barua pepe: rbcsongwe@pccb.go.tz**

**Wavuti: http://www.pccb.go.tz**

## TAARIFA YA KAZI ZA TAKUKURU MKOA WA SONGWE KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI 2016 – MACHI 2017

**Ndugu Wanahabari**

Napenda nichukue fursa hii kuwashukuruni wote kwa kuitikia wito wetu, pia niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya ya kutoa habari na kuelimisha umma. Nimekuiteni tuzungumze kuhusu mapambano dhidi ya rushwa katika mkoa wetu wa Songwe wenye wilaya nne yaani Mbozi, Momba, Ileje na Songwe. Mazungumzo haya yanalenga kuuhabarisha Umma kuhusu mapambano dhidi ya rushwa katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017. Taarifa ya mapambano haya ni muhimu iwafikie wananchi ili wazidishe ushirikiano wao katika kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI ya kukabiliana na tatizo la rushwa. Kauli na vitendo vya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Urais, wakati akilihutubia Bunge na katika kipindi chote hiki cha uongozi wake vinadhihirisha azma hii.

**Ndugu Wanahabari**

Napenda kuwakumbusha kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ndicho chombo kilichopewa dhamana kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007 kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Kwa mujibu wa Sheria hii, TAKUKURU imepewa majukumu makuu matatu:

1. Kuzuia rushwa kwa kufanya tafiti mbalimbali pamoja na uchambuzi wa mifumo yenye lengo la kuziba mianya ya rushwa,
2. Kuchunguza na kuwashtaki mahakamani watuhumiwa wanaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa kwa mujibu wa sheria,
3. Kuelimisha Umma uichukie rushwa na kuyatambua madhara yake na hivyo kuongeza ushiriki wa wananchi wote katika mapambano dhidi ya rushwa.

**Ndugu Wanahabari**

Kwa upande wa kuzuia rushwa katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoa wa Songwe imefanya utafiti na uchambuzi wa mifumo **05,** kazi hizi ziko katika hatua za mwisho ambapo idara husika zitashauriwa namna ya kuziba mianya ya rushwa na kuweka mikakati inayopimika ya kudhibiti mianya ya rushwa iliyobainika, pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikakati itakayowekwa. Tafiti na chambuzi za mifumo zilizofanyika ni:-

- Mianya ya Rushwa katika Hospitali ya Misheni Mbozi
- Mianya ya Rushwa katika mitihani ya kidato cha nne, 2016
- Mianya ya Rushwa katika upatikanaji na utoaji wa huduma za afya katika kituo cha afya Tunduma
- Mianya ya Rushwa katika upimaji wa magari ya uzito na abiria katika mizani ya Nkangamo - H/W Momba pamoja na Mpemba H/Mji Tunduma
- Mianya ya Rushwa katika ugawaji wa ardhi katika vijiji H/W - Ileje

Aidha katika kipindi hiki, jumla ya miradi ya maendeleo **08** yenye thamani ya **TZS 1,477,625,463/=** ilikaguliwa. Baadhi ya miradi hiyo ilibainika kuwepo kwa vitendo vya udanganyifu katika matumizi ya fedha za Serikali, uchunguzi umeanzishwa na unaendelea. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na:-

- Mradi wa skimu ya umwagiliaji Naming'ong'o H/W Momba uliogharimu zaidi ya TZS 600,000,000/=
- Mradi wa Mji katika kijiji cha Lukululu H/W Mbozi uliogharimu jumla ya TZS 189,000,000/=

- Mradi wa ukarabati wa maghala 11 uliogahrimu jumla ya TZS 688,625,463; Ghala la Hantesya na Old Vwawa TZS 117,765,796; Ghala la Itumpi na Msanyila TZS 135,994,426; Ghala la Nansama TZS 71,738,730; Ghala la Ibembwa na Nambinzo TZS 117,330,332; Ghala la Wasa naRuanda TZS 119,341,845; Ghala la Iyula na Ilomba TZS 126,454,335.

**Ndugu Wanahabari**

Kwa upande wa uchunguzi na mashitaka katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017, tulipokea jumla ya taarifa 74 za malalamiko ya vitendo vya rushwa. Kwa mujibu wa taarifa hizo, Idara zinazoongoza kwa kulalamikiwa ni Serikali za Kata/Vijiji/Mitaa/Kitongoji (14), Afya (09), Polisi (09), Mahakama (08), Elimu (06) Vyama vya Ushirirka (03), Mabaraza ya Usuluhishi (02), Utawala (02), TANROADS (02), Ukusanyaji Ushuru (02), Ujenzi (02), Usafirishaji (1), Kilimo (01), Uvuvi (01), Zimamoto (01), Michezo (01), Mipango (01), Wanyamapori (01), Vyama vya Siasa (01), Ugavi (01), Maliasili (01), Uhamiaji (01), Ardhi (01), TASAF (01) na NGOs (01).

Katika kipindi hicho, tumefanikiwa kuchunguza na kukamilisha majalada **21** ambayo yamewasilishwa katika Mamlaka husika kwa maamuzi ya kisheria. Idara zilizofanyika chunguzi hizo ni Idara ua Utawala (08); Afya (03); Ujenzi (02); Elimu (02); Mahakama (01); Polisi (01); Vyama vya Siasa (01); Forodha (01); TASAF (01) na Ugavi (01). Aidha, katika kipindi hiki tumeweza kuokoa fedha taslim za Serikali kiasi cha **TZS 11,183,000.00** ambazo zilikuwa mikononi mwa watu binafsi pamoja na Taasisi. Fedha hizi zimeingizwa kwenye akaunti maalum ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU ambayo inahifadhi fedha zinazookolewa ili ziweze kuwasilishwa Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli nyingine zitakazokuwa na tija kwa wananchi wote.

Vile vile tumefanikiwa kufungua kesi **01** katika Mahakama ya Wilaya ya Momba iliyopo eneo la Chapwa katika Mji wa Tunduma. Kesi hiyo ni namba **CC 21/2017 Jamhuri v THADEI DAUD NYONI**, mtumishi wa TANROADS ambaye ni 'Shif in Charge' wa Kituo cha Mzani Mpemba aliyeomba na kupokea rushwa ya TZS 100,000.00 mwezi Januari mwaka 2017 kinyume na Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na

Rushwa Na. 11/2007. Aidha, tayari tumepata kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) cha kufungua kesi nyingine **01** katika Mahakama ya wilaya ya Ileje yenye tuhuma katika Idara ya Utawala na Ugavi ambapo taratibu za kufungua kesi hiyo zinaendelea.

Kwa mara nyingine tena napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha watumishi wa umma hususan katika Idara zinazoongoza kwa kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa watekeleze majukumu yao kwa weledi na uaminifu ili kutoweka rehani mustakabali wa utumishi wao.

**Ndugu Wanahabari**

Katika uelimishaji Umma kuhusu rushwa na madhara yake kwa kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017, tuliimarisha Klabu 55 za wapinga rushwa katika shule za Sekondari, tulifanya mijadala ya wazi 08, tulifanya semina 33, tuliandaa na kurusha vipindi vitatu (3) vya Radio na tulishiriki maonesho matano (5). Kutokana na kuelimisha Umma, tumekuwa tukipokea taarifa nyingi kutoka kwa wananchi kutujulisha vitendo vya rushwa na ufisadi ndani na nje ya mkoa wetu. Nawaomba wananchi waendelee na moyo huo wa ushirikiano kwa TAKUKURU.

**Ndugu Wanahabari**

Taasisi ya Kuzuia Rushwa mkoani Songwe tumejipanga kuondoa kero kwa wananchi hasa katika maeneo yanayolalamikiwa kwa kuwachunguza watumishi wa umma na kuwafikisha Mahakamani pale wanapobainika kufanya vitendo vya rushwa, kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu rushwa na wajibu wao katika mapambano dhidi ya rushwa, na kubaini na kudhibiti mianya ya rushwa kupitia utafiti na uchambuzi wa mifumo.

Aidha, TAKUKURU mkoa wa Songwe tumejielekeza katika kukagua miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuokoa fedha za serikali na kuchukua hatua za kisheria kwa watumishi wanaobainika kuihujumu miradi hiyo. Wale waliodhani kuwa fedha za miradi hiyo ni za kuchota kama maji ya mtoni watambue kwamba hawako sahihi na Taasisi itawashughuikia bila kujali vyeo vyao wala upendeleo wa aina yoyote ile.

Natoa wito kwa wananchi wote katika mkoa wa Songwe waendelee kutuunga mkono katika mapambano haya kwa kukataa kutoa na kupokea rushwa na pia kuwafichua wale wote wanaoendekeza vitendo vya rushwa.

Ninakushukuruni nyote kwa kuja na kunisikiliza na ninaamini mtaifikisha taarifa hii kwa wananchi na watumishi wa umma ili watambue wajibu wao katika mapambano haya adhimu kwa ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Taifa letu.

***Jaspar P. Mmbaga***
***Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe***
***Aprili 18, 2017.***